OFISI YA RAISI-TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

SHULE YA SEKONDARI TUMATI

S.L.P 197,

MBULU.

18/6/2018

KUMB.NA.TSS/HOS/ADM/KDT/V/2018 SIMU: 0786096939/062905752

JINA LA MWANAFUNZI……

S.L.P…….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI TUMATI,MWAKA 2018.

1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi sana na kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga katika shule ya sekondari Tumati kwa masomo yako ya kidato cha tano katika tahasusi(combination)……. Kwa mwaka wa masomo 2018/2019. Kwa barua hii nakukaribisha na kukuarifu kuwa masomo yataanza tarehe 16/7/2018, hivyo unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe 15/7/2018 na mwisho ni tarehe 30/7/2018,Unatakiwa kuripoti kwa Makamu Mkuu wa Shule ili usajiliwe na baada ya tarehe ya mwisho ya kuripoti utakuwa umepoteza nafasi hiyo.

2.0. MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Tumati ipo katika kata ya Tumati Mkoa wa Manyara,Halmashauri ya wilaya ya Mbulu na Tarafa ya Dongobeshi.

Umbali wa shule kutoka makao makuu ya Tarafa ya Dongobeshi hadi shuleni ni kilometa saba (7Km).

Usafiri wa kufika shuleni, Usafiri ni wa mabasi nyakati za jioni na asubuhi,Wanafunzi wanaotoka sehemu mbalimbali mwa Tanzania watumie mabasi ya Babati hadi Dongobeshi stendi halafu mabasi yaendayo Tumati, Pia kutoka Arusha-Karatu-Mbulu-Dongobeshi stendi atafute mabasi ya Tumati hadi shuleni . Vilevile toka Singida- Haydom-Dongbesh stendi halafu magari yaendayo Tumati.

KWA MAWASILIANO ZAIDI: 0786096939/ 0683905626

3.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

Mazingira ya Shule ya Tumati ni ya hali ya ubaridi nyakati za miezi ya Machi hadi Julai hivyo mwanafunzi avae nguo za kujikinga na baridi.

3.1 SARE ZA SHULE

- Sketi mbili za dark blue kitambaa kizito Rinda (Boksi) na urefu ni Sm 10 kutoka kwenye goti.
- Blauzi mbili nyeupe mikono mirefu
- Sweta moja rangi ya dark blue
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba ,visiwe na kisigino kirefu (Jozi mbili).
- Singland nyeupe, na Soksi nyeupe pea mbili
- Tai dark blue.

SARE KWA WANAFUNZI WA DINI YA KIISLAMU

Mwanafunzi wa kiislamu wanapaswa kuvaa hijabu kulingana na maadili ya dini yao na si vinginevyo na sketi mbili za rangi ya dark blue , hijabu nyeupe isiyo na Urembo wa aina yoyote.

NB: - Mwanafunzi akijishonea kinyume na maelezo ya mashono hatopokelewa.

- Mwanafunzi hatoruhusiwa kuja na nguo za nyumbani bali na vitu alivyoagizwa tu.
- Siku ya kuripoti awe amevaa sare sahihi ya shule.
- Hatoruhusiwa kwenda Bwenini kama hajakamilisha usajili
- Mwanafunzi haruhusiwi kusuka hata kama amevaa hijabu.
- Mtu yeyote haruhusiwi kumtembelea mwanafunzi Bwenini.
- Mzazi/Mlezi anaruhusiwa kumtembelea mtoto wake siku ya jumapili ya mwisho wa mwezi na ukifika shuleni pitia mapokezi kwa maelezo zaidi.

3.2. SARE ZA MICHEZO

- T-Shirt ya blue moja.
- Skirt fupi ya blue(mtindo wa mwamvuli) na skin tight ndefu nyeusi.
- Raba za blue (Jozi moja).

3.3. MAHITAJI YA BWENI

- Godoro size 2½ X 3 X 6.
- Shuka 2 (Blue 1 na Pink 1.)
- Blanketi 1,mto na foronya la blue na pink.
- Tranka 1.
- Ndoo 2 ndogo

- Traki nyeusi 1 na shamba dress(Skirt light blue kitambaa kizito)
- Ndala za kuogea.

3.4. MAHITAJI YA DARASANI

- Madaftari ya counter books (Q3) = 10
- Madftari madogo ya mazoezi
- Mkebe wa hesabu (Mathematical Set) =1
- Begi la kubebea daftari na vitabu.
- Kalamu,Penseli za kutosha,Rula na Kifuto.

3.5. VYOMBO VYA CHAKULA

- Sahani 1 na Bakuli viwe vya mifupa
- Kijiko 1.

4.0.CHAKULA CHA WANAFUNZI

Wanafunzi wa bweni chakula chao kinalipwa na Serikali kuu Ofisi ya Raisi –Tamisemi

5.0 ADA NA MICHANGO MINGINE

Shule ya Tumati Sekondari ina wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha Tano.Hivyo kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne hawalipi ada na michango mingine.

Kidato cha Tano na sita wanalipa ada ya shule shilingi Tsh, 70,000/= kwa mwaka na mzazi au Mlezi anaweza kulipa kwa awamu (Muhula) Tsh 35,000/= kupitia Benki.

Michango mingine ni kama ifuatavyo;-

- FEDHA ZA TAHADHARI - 5,000/= (Ambayo haitarudishwa) Mara moja
- MATIBABU- =6,000/= Kwa mwaka
- UBORESHAJI WA TAALUMA - 20,000/= Kwa mwaka
- HUDUMA YA KWANZA-10,000/=Kwa mwaka
- MISHAHARA YA WAPISHI NA WATUMISHI WENGINEO -30,000/= Kwa mwaka
- SAMANI- 15,000/= Kwa mwaka
- MITIHANI YA UTAMIRIFU (MOCK)- 20,000/= Kwa Mwaka
- NEMBO – 2,000/= Mara moja
- KITAMBULISHO NA PICHA - =6,000/= Mara moja

N:B 1. Kwa wale wenye Bima ya afya waje na kadi ya Bima na wasilipe fedha za matibabu.

2.Fedha zote zilipwe katika benki ISIPOKUWA FEDHA ZA MATIBABU NA FEDHA ZA TAHADHARI

AKAUNTI YA SHULE NI N.M.B A/C NO 4121200078,

JINA LA AKAUNTI NI TUMATI SEKONDARI.

3. Ukifika shuleni wasilisha “bank pay in slip kwa Mhasibu wa shule”

6.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE ZA SEKONDARI.

Shule zote za sekondari Tanzania zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na Marekebisho yake ya Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha shule inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara ya Elimu ,Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Raisi- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

6.1. **Mambo yanayopaswa kuzingatiwa na ya msingi kwenye sheria na kanuni za shule.**

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka. Hivyo huruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa maalumu.

f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.

g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

i) Kutunza mali za umma.

6.2**. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule**

i) Wizi ii)Uasherati,Ubakaji na Ushoga.

iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya

Iv) Uvutaji wa bangi V) Makosa ya jinai Vi) Kupigana au kupiga. Vii) Kuoa au kuolewa

Viii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma Ix) Kudharau Bendera ya Taifa

X) Kupata Mimba au Kusababisha Mimba ndani na nje ya shule.

Xi) Kutoa Mimba Xii) Kugoma ,Kuchochea na Kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa

Watu Xiii) Kukataa adhabu kwa makusudi

Xiv) Kumiliki simu ya mkononi kwa namna yeyote ile bila kibali maalumu.

NB: Unatakiwa kuzingatia mambo ya muhimu ya msingi katika sheria za shule na utafafanuliwa kwa undani mara baada ya kuripoti shuleni.

MAMBO YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI MARA ANAPORIPOTI SHULENI.

1. Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya serikali/au Hospitali nyingine zinazotambuliwa na serikali.
2. Fomu ya mwanafunzi kukiri na kutoa ahadi ya utii muda wote atakapokuwa shuleni.
3. Fomu ya Mzazi/Mlezi kukubali kushirikiana na Uongozi wa shule katika malezi ya mtoto wake.
4. UNAPORIPOTI UNATAKIWA KUJA NA BARUA YA MAAGIZO (JOIN INSTRUCTIONS) ILIYOJAZWA KIKAMILIFU, VYETI VYAKO VYA TAALUMA (RESULT SLIP NA CHETI CHA KUZALIWA).

Ahsante

Karibu sana Shule ya Sekondari Tumati.

…….

Mkuu wa Shule.

KILIAN JOHN

7.0. **FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA AU HOSPITALI NYINGINE ZINAZOTAMBULIWA NA SERIKALI, NA MWANAFUNZI AJE NA HII FOMU PINDI ANAPORIPOTI.**

Mimi/ Jina la Mganga……..

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la Mwanafunzi……..

Amepima kikamilifu na kuonenaka kuwa ana/hana afya nzuri kwa mujibu wa Taarifa zifuatazo;-

A. HALI YA MWILI
   i. Mapigo ya moyo……
   ii. Haemaglobin HB……
   iii. Kundi la damu (Blood Group)……..
   iv. Mkojo (Urine)……..
   v. Kinyesi (Stool)……..
   vi. Macho (yana kasoro) Eye test……..
   vii. Masikio (yana kasoro)……
   viii. Ujauzito (Check Cases of Pregnancy)……
   Angalia ;- Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (i-viii)
   ……
   ……
   ……

B. MAGONJWA
   Amewahi/ hajawahi/ana/hana/magonjwa yafuatayo-;
   a. Pumu (Arthma)…….
   b. Kifua Kikuu (TB)……..
   c. Kifafa(Epilepsy)…….
   d. Shinikizo la damu la juu/chini(Blood pressure)……
   e. Vidonda vya Tumbo (Ulcers)……..
   f. Maradhi ya zinaa…….
   g. Ukoma (Leprosy)……..
   h. Ugonjwa wa akili (Mental illness)…….
   i. Maradhi mengineyo makali ambayo hayajatajwa hapo juu kama yapo……
   ……

……..
Tarehe……

NB: KATA ISIYOHUSIKA

7 B**. FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI KUKIRI NA KUTOA AHADI YA UTII YA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi…….Wa kidato cha ……Mwaka……
Nimesoma na kuelewa fomu na maagizo yaliyoambatanishwa juu,utaratibu, kanuni za shule na sheria zake. Endapo nitapatikana na makosa yanayohusiana na vifungu vilivyoorodheshwa kwenye fomu ya kujiunga na shule hii, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu kulingana na vifungu hivyo muda wote niwapo shuleni ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

…… ……..
Saini ya mwanafunzi Saini ya Mkuu wa Shule
Tarehe…… Tarehe…….

7.C **FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKUBALI KUSHIRIKIANA NA UONGOZI WA SHULE**.

Mimi …….Mzazi/Mlezi wa ……
Nimesoma na kuelewa maagizo yaliyotolewa na uongozi wa shule.Nina kubali na ninaahidi kutekeleza maagizo yaliyotolewa,Vilevile nitatoa ushirikiano kwa uongozi wa shule kwa malezi ya watoto wangu.

……..
Saini ya Mzazi/Mlezi
Tarehe…….